# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba Mbingu na Ardhi na Vilivyomo ndani yake kwa kutuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la Wawakilishi Zanzibar kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba na kisheria ya kuwawakilisha wananchi kupitia chombo hiki.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, nakushukuru na kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti kwa namna mnavyoliongoza na kuliendesha Baraza hili kwa umahiri mkubwa. Ninamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishieni hekma na busara katika majukumu yenu ya kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wetu.

**Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii pia kushukuru uongozi mzima wa Baraza unaoongozwa na Katibu wa Baraza ndugu Raya Issa Msellem pamoja na watendaji wa Baraza kwa mashirikiano yao makubwa wanayoyatoa kwa Kamati yetu katika kuhakikisha kuwa Kamati inatekeleza vyema na kwa ufanisi majukumu yake ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, pongezi za pekee ziende kwa Waziri wa Katiba

na Sheria na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa mashirikiano waliyotuonesha katika utekelezaji wa kazi zetu, Tunawatakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yao na wazidishe mashirikiano na Kamati kwa lengo la kupata ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inawasilisha Ripoti hii kwa kutimiza masharti ya Kanuni ya *109(14)* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, ambayo inaitaka kila Kamati kutayarisha ripoti ya mwaka itakayowasilishwa katika kikao cha mwezi wa Februari cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kanuni ya *109(15)* ya Kanuni za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa mapendekzo hayo, Kamati inatakiwa kukaa na Wizara husika kujadili utekelezaji huo. Kamati, katika kutekeleza hili ilikutana na Wizara na Taasisi ambazo zilipewa maagizo au ushauri chini ya mwamvuli wa Wizara ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inalenga utekelezaji wa Ushauri na Maoni au Mapendekezo kwa Kamati kwa Wizara na Taasisi zifuatazo:

(a) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.
(b) Wizara Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.
(c) Wizara ya Fedha na Mipango.
(d) Wizara ya Afya.
(e) Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni, na Michezo.
(f) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali .
(g) Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na uchukuzi.

## UTEKELEZAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefarijika na inazipongeza Wizara na Taasisi zote ambazo zimetekeleza Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwani kufanya hivyo kunaimarisha utendaji na utoaji wa huduma katika Taasisi zao.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Wizara Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ya kuratibu taarifa za utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa Wizara mbali mbali ambapo Kamati inapongeza taasisi ambazo zimepewa maagizo hayo na kuyatekeleza.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa hatua hizo zilizofikiwa ni pamoja na:
Baadhi ya Kanuni kutangazwa upya baada ya marekebisho ambayo yamezingatia miongozo ya Kamati
Baadhi ya Kanuni zipo katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa lengo la kufanyiwa Mapitio na nyengine zipo ambazo zinasubiri Marekebisho ya Sheria husika ili ziweze kwenda sambamba.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, licha ya juhudi hizo zilizochukuliwa bado kuna maoni na mapendekezo kadhaa ya Kamati yanaonekana kuwa ndio yanaendelea kufanyiwa kazi. Kamati inasisitiza kuwa Taasisi zote zilizopewa mapendekezo ushauri na maoni kuchukuwa hatua za haraka kuteleza mapendekezo hayo, kwani Kamati ya Kanuni ndio msimamizi Mkuu wa Utekelezaji kwa niaba ya Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa Mapendekezo hayo ni kuongeza uwezo wa watendaji wanaohusika na uandishi wa Kanuni katika Taasisi na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwani Kanuni nyingi zilizowasilishwa zimebainika kuwa

na kasoro za kiuandishi.

**Mheshimiwa Spika,** Baadhi ya Kanuni zilizobainika kuwa na kasoro zilitakiwa kurekebishwa na kuwasilishwa tena katika Kamati. Zikiwemo zile zilizowasilishwa kwa lugha ya Kiingereza na kutakiwa kuwasilishwa kwa lugha ya kiswahili.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, kuna Kanuni ambazo ziliwahi kuwasilishwa hapa barazani kwa lugha ya kiengereza ambazo Kamati iliagiza zikaandikwe kwa lugha ya Kiswahili hazijarejeshwa tena. Mfano wa Kanuni hizo ni Kanuni za Bodi ya Chakula Dawa na Vipodozi. Kamati inashindwa kuelewa kuwa Taasisi hiyo inafanya kazi kwa utaratibu gani huku ikiwa Kanuni hizo bado hazijakamilika kwa kupata maoni na ushauri wa kisheria wa Kamati hii ya Kanuni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kusisitiza utungaji wa Kanuni kwa lugha ya Kiswahili, maelekezo haya Wizara ya Katiba na Sheria iliyachukuwa na kuyafanyia kazi. Hata hivyo, changamoto inayojitookeza baadhi ya Taasisi zinawasilisha Tafsiri ya Kanuni Badala ya Kuandika Kanuni mpya kwa lugha ya Kiswahili.

Hivyo; Kamati inasisitiza Wizara kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu kutoa miongozo juu ya Utaratibu kwa kuwasilisha Kanuni mpya badala ya kuwasilisha Tafsiri za Kanuni.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia Hotuba yangu hii fupi naomba nitumie nafasi hii kuikumbusha Serikali kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Tume ya Kurekebishi Sheria, ambazo zote zipo chini ya Wizara ya Katiba na

Sheria kuhusu umuhimu na uharaka wa kuifanyia marekebisho au kuitunga upya Sheria ya Ufafanuzi namba 7/1984 (**The Interpretation of Laws and General Provisions Act, 1984).** Suala hilo limesisitizwa na Kamati hii kwa nyakati tofauti bila ya kuonekana kupewa uzito unaostahiki katika utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii imetungwa na Baraza hili la Wawakilishi mnamo tarehe 10 Oktoba, 1984 na ndiyo Sheria inayotoa muongozo wa ufafanuzi, utumiaji wa Sheria zote zinazotungwa na Baraza hili. Sambamba na hilo, Sheria hii imeweka ufafanuzi na miongozo ya namna gani Sheria Ndogo Ndogo zinapaswa kutungwa na kutumika. Hata hivyo, Sheria hii imekuwa ya zamani sana na inahitaji kurekebishwa au kutungwa upya kwa vile masharti mengi yaliyomo yanahitaji kuimarishwa zaidi kwa mfano vifungu vinavyozipa uwezo Sheria Ndogo kuweka adhabu kwa atakayekiuka masharti ya Sheria hizo, kama vile kifungu cha 42 (e) cha Sheria hiyo kimetoa uwezo wa kuwekwa faini isiyozidi shilingi elfu saba ambayo kwa wakati wa sasa ni faini ndogo sana.

**Mheshimiwa Spika,** nimesema nilikumbushie suala hili kwa vile lishawahi kuripotiwa katika taarifa zetu zilizotangulia katika Baraza hili. Hivyo ni vyema nikawakumbusha wenzetu wa Wizara baadhi ya vitu vya msingi vya kwenda kuvifanyia kazi ambavyo tumevishauri pamoja na kuhakikisha kwamba Sheria zote zilizokwisha kupitishwa ndani ya Baraza hili hivi karibuni ambazo hazina Kanuni zihakikishwe zinatungwa na Mmalaka husika na kuwasilishwa Barazani kwa lengo la kupitiwa na Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa msingi wa kufuata utaratibu ili dhamira ya kukasimiwa madaraka Waziri au Mkuu wa Taasisi kutunga Kanuni husika ifikiwe na kuona kwamba zinakidhi kutumika kwake kwa

mujibu wa Sheria na kuzingatia mipaka ya kisheria husika.

**Mheshimiwa Spika,** si jambo baya tukitunga taratibu zinazotumiwa na Mamlaka nyengine wakati wa kutunga Sheria ambapo Mswada wa Sheria unapowasilishwa Barazani ikiwa Sheria hiyo inahitaji Kanuni katika utekelezaji wake, rasimu ya Kanuni hiyo huwa tayari imeshaandaliwa na inasubiri mchakato wa kukamilika Sheria ili nayo iweze kutangazwa, kufanya hivyo kunaweza kutuepusha na changamoto nyingi zinazotokana na kuchelewa kutungwa kwa Kanuni.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa, nachukuwa fursa hii kuzitaka Wizara na Taasisi zote za Serikali ambazo Kanuni zao zitapitiwa na Kamati hii, kutoa mashirikiano kwa Wizara ya Katiba na Sheria wakati wa kutayarisha taarifa ya utekelezaji wa maelekezo ya Kamati yanayotolewa kwa Wizara au Taasisi hizo, jambo hili ni muhimu kwa vile lipo kikanuni.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii tena kuishukuru Wizara Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mashirikiano yake inayoipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake na pia niombee kwa Allah kuzidisha mashirikiano hayo ili kuweza kufikia lengo la Serikali katika kuleta maendeleo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, shukrani za dhati ziende kwa Mhe. Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ pamoja na timu yao nzima ya wataalamu kwa kutekeleza vyema na kwa uharaka maoni, mapendekezo na ushauri wa Kamati kwa kuweka misingi bora ya matumizi ya Sheria Namba 7 ya 2014.

**Mheshimiwa Spika,** Kasi hii kama ingeigwa na Taasisi zote za Serikali basi tungekua na Kanuni bora na zenye kutekelezeka.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mfupi Wizara imeratibu vyema utungwaji wa Kanuni za Usafi na Adhabu za Papo kwa Papo kwa Manispaa na Halmashauri zote Zanzibar, ili kuzidisha usafi katika miji yetu na kupunguza mzigo wa kesi katika Mahkama za mwazo. Hatahivyo, bado naomba kusisitiza kwa Wizara ya Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kusimamia majadiliano kati ya Mahkama na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhusu mapato yanayotokana na faini mbali mbali chini ya Kanuni hizi yabaki katika Mamlaka husika ili kusaidia kunyanyua na kuimarisha Miji yetu kuendana na maagizo ya Mhe. Rais wa Zanzibar katika suala zima la usafi na kuimarisha haiba ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uhalisia wa majukumu ya Kamati yetu ni Kamati ya kitaalamu na inatakiwa kutekeleza majukumu yake kwa kupitia kazi zilizokwisha kufanywa na wataalamu. Hivyo, kuna haja ya kuchukua jitihada za makusudi na kupewa uzito Kamati hii, juu ya suala la kujengewa uwezo hasa katika fani ya uandishi na uchambuzi wa Sheria na Kanuni ili iweze kufanya kazi zake ipasavyo, ni vyema Kamati ikapata fursa ya kwenda kujifunza katika Mamlaka nyengine ili kupata uzoefu wa mabunge tofauti katika utendaji wa kazi zake.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa mashirikiano makubwa ya dhati kabisa katika kutekeleza majukumu ya Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuondoka katika kipaza sauti hiki naomba niwashukuru na kuwatambua kwa majina Wajumbe wote wa Kamati na Wasaidizi wao kwa ushirikiano wao unaopelekea ufanisi wa Kamati hii

Wajumbe hao ni:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Mihayo Juma N'hunga | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Zawadi Amour Nassor | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Mohamed Ahmada Salum | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Kombo Mwinyi Shehe | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Issa Haji Ussi | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati yetu ina Makatibu *wawili (2)* kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi, ambao wanaratibu shughuli zote za Kamati hii ambapo wanatoa mashirikiano makubwa yanayopelekea ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yetu. Kwa ruhusa yako, naomba niwataje majina yao kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| *1.* | Ndugu Karima Abdul-Wahab |
| *2.* | Ndugu Abdu Maulid Haji. |

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Ahsante,

…………………………….
**(**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**)**
Mwenyekiti,
Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**